TAMBUA HAKI ZAKO:
UZUIAJI, UCHUNGUZI NA MATIBABU YA KIFUA KIKUU

HAKI ZAKO ZA KIBINADAMU NA TB

NA GISA DANG

Imehaririwa na Tsira Chakhaia, Brian Citro, Vivian Cox, Mike Frick, Jennifer Furin, Erica Lessem, Alexander William Mbuya, Lindsay McKenna, John Mdluli, Jane Rahedi Ong'ang'o, Hadija H. Semvua, na Zani de Wit

Ukurasa wa 1 kati ya 6

Kwa nini tumetoa mwongozo huu?

Mwongozo huu ni kwa watu wenye kifua kikuu (TB), watu walio katika hatari ya kuambukizwa TB, na waangalizi wao. Unakusudia kuelezea vipi viwango vya ulimwengu vya huduma ya TB, ikijumuisha huduma unayopaswa kupokea. Mwongozo huu unakusudia kuelezea kwa ufasaha haki zako zinazohusiana na uzuiaji, upimaji, matibabu na uangalizi wa TB. Lengo letu ni kwa watu walioathiriwa na TB kuweza kutambua ni lini wanapaswa kupokea uangalizi wa hali ya juu, ili waweze kuomba viwango vilivyopendekezwa vya ulimwengu.

Viwango vya ulimwengu vilivyopendekezwa ni vipi?

Shirika la Afya Duniani (WHO) ni Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) linalojihusisha na afya. Sehemu ya kazi ya WHO ni kuongoza mchakato unaoweka viwango na miongozo ya uzuiaji, uchunguzi, na matibabu ya TB. Viwango hivi vinawasaidia waundaji wa sera na mamlaka za afya kupanga na kuziwezesha programu za nchi zao kuheshimu, kulinda na kutimiza haki za kila mtu za afya na haki zingine za kibinadamu.

Je, Haki za Binadamu ni nini, na kwa nini ni za muhimu kwa watu walioathiriwa na TB?

Watu wenye TB na walio katika hatari ya kupata TB wana haki za kibinadamu. Chini ya sheria za kimataifa, kikanda na za ndani, serikali zinatakiwakuheshimu, kulinda na kutimiza haki hizi za binadamu. Haki za binadamu ni suala la ulimwengu wote: kila mtu anazo. Haki za binadamu pia haziwezi kugawanywa, zinategemeana zote na zinahusiana mahali kote. Hiyo inamaanisha haki zote za binadamu ni za muhimu kwa usawa, zinategemeana na zinahusiana. Kuondoa haki moja kunaathiri haki zako nyingine.

Haki nyingi za binadamu ni za muhimu kwa watu wenye TB. Haki hizi zipo kulingana na makubaliano ya kimataifa na kikanda, pamoja na katiba za nchi duniani kote. Zinajumuisha Haki ya Kuishi; Haki ya Afya; Haki dhidi ya Ubaguzi; Haki ya Uhuru; Haki ya Sayansi; Haki juu ya Ridhaa ya kutaarifiwa; Haki ya Taarifa; Haki ya Faragha; Haki ya Ushirikishwaji; Uhuru dhidi ya Unyanyasaji na Mateso, Ukatiki au Vitendo vya Uonevu; Uhuru wa Kutembea, Uhuru dhidi ya Vizuizi vya Udhalimu; Uhuru wa Kuungana; na Uhuru wa Kukusanyika.

DR-TB STAT

TAG Treatment Action Group
www.treatmentactiongroup.org

Januari 2018

Je, Haki ya Kuishi inamaanisha nini kwa watu walioathirika na TB?

Haki ya Kuishi inamaanisha kwamba nchi, yaani, serikali ya nchi yako, haiwezi kukunyima kuishi. Nchi pia ina wajibu wa kuchukua hatua kulinda maisha yako. Hii inamaanisha serikali yako inatakiwa kuchukua hatua kukomesha magonjwa na kuhakikisha upatikanaji wa huduma, kwa mfano kwa kuchukua hatua zinazohusiana na haki za binadamu kutokomeza TB.

Je, Haki ya Afya inamaanisha nini kwa watu walioathirika na TB?

Haki ya Afya inahusisha sehemu mbili muhimu. Sehemu ya kwanza ni huduma za afya za nchi na mfumo wa huduma za afya. Haki ya Afya inasema kuwa huduma ya afya inapaswa kuwa inapatikana. Kwa TB, hii inamaanisha mfumo wa huduma ya afya wenye nyenzo zinazofanya kazi ili kuhakikisha uzuiaji, utambuzi na matibabu ya TB; kwa vifaa ikijumuisha vifaa vya matibabu na kupimia; na huduma na programu ikijumuisha bajeti ya kutosha kwa ajili ya wafanyakazi wanaotoa huduma ya afya pamoja na mipango ya TB. Huduma za afya zinatakiwa ziwe zinapatikana: kila mtu anapaswa kuzipata na hawezi kukatazwa kuhudumiwa (kitendo kinachoitwa kutobagua). Pia unapaswa kuwa na uwezo wa kufika na kuingia katika vituo vinavyoweza kudhibiti TB, ikijumuisha, kwa mfano, vituo vya karibu vya huduma za afya, au, ikibidi, huduma zinaweza kuletwa ulipo. Unapaswa kuwa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya huduma za afya, ikijumuisha matibabu. Na unatakiwa uwe na uwezo wa kupata taarifa kuhusiana na chaguzi za huduma za afya zipatikanazo kwa ajili ya TB na ufahamu juu ya TB. Huduma ya afya inapaswa kukubalika; hii inamaanisha kuwa huduma ya afya inapaswa kuwa inayofaa tamaduni ya eneo hilo, inayoheshimu utu, inayojali jinsia na umri wa mtu mwenye TB. Huduma ya afya inapaswa kuwa yenye ubora wa juu: matibabu ya TB yanapaswa kuwa yanayozingatia sayansi na yanayofaa kimatibabu, na dawa zinapaswa kuwa zenye ubora wa juu.

Sehemu hii ya "upatikanaji, ufikiaji, ukubalikaji na ubora" ya haki ya afya mara nyingi huitwa AAAQ.

Sehemu ya pili ya Haki ya Afya inajumuisha "vibainishi vya msingi" vya afya. Hivi vinajumuisha haki mbalimbali za binadamu zinazohusiana na afya yako. Kwa mfano, haki ya chakula; maji safi na salama, usafi wa kutosha; makazi ya kutosha; hali nzuri za kazi; na upataji wa elimu ya afya. Haki hizi ni muhimu katika uzuiaji na matibabu ya TB. Kwako wewe, hili linaweza kumaanisha kwamba unapaswa kupokea usaidizi wa virutubisho ukiongezea dawa wakati wa matibabu ya TB, ikiwa hiyo itasaidia uponaji wako. Au kwamba unaweza kuhitaji usaidizi zaidi wakati au baada ya kuwa umemaliza matibabu yako, ikiwa TB imebadilisha kwa kiwango kikubwa hali yako ya jinsi unavyoishi na kulinda afya yako.

Pia serikali yako inatakiwa itoe dawa muhimu. Huu ni "wajibu mkuu" chini ya Haki ya Afya. Hii inamaanisha kwamba kutoa dawa za muhimu ni moja ya vitu muhimu serikali inaweza na inatakiwa kufanya ili kuheshimu, kulinda na kutimiza Haki ya Afya. WHO ina Orodha ya Dawa Muhimu, inayoorodhesha dawa zote muhimu za TB katika sehemu ya 6.2.4 ya toleo la 19.

Je, Haki dhidi ya Ubaguzi inamaanisha nini kwa watu walioathirika na TB?

Hali yako ya afya haipaswi kutumiwa kama sababu ya kukutendea wewe, familia yako au mtu anayekuhudumia kwa namna yoyote tofauti na wengine. Hii inamaanisha kwamba huwezi kufukuzwa kazi, kukatazwa kujiunga na shule, kukatazwa makazi au kukosewa heshima katika kliniki ya afya kwa sababu una TB. Ikiwa wewe ni mshirika wa kundi lililohatarishwa, kwa mfano mtu mwenye HIV, mtu atumiaye dawa haramu, mkimbizi au mfungwa, hupaswi kubaguliwa unapojaribu kupata huduma za TB.

Je, Haki ya Uhuru, Uhuru wa Kutembea, Uhuru dhidi ya Kuzuiliwa Ovyo vinamaanisha nini kwa watu walioathirika na TB?

Haki hizi zinakuhakikishia kuwa huwezi kufungwa, kuwekwa kizuizini au kukatazwa kukutembea bila taratibu za kisheria. Kuzuiliwa ama kukamatwa kokote kunapaswa kufanywa kulingana na sheria. Hii ni muhimu kwa TB tunapofikiria kuhusu iwapo matibabu yanapaswa kufanywa mtu akiwa ametengwa. Kutengwa wakati wa matibabu ya TB kunaweza kufanywa ikiwa kunahitajika kimatibabu ili kuwaepusha wengine dhidi ya TB. Hata hivyo, unapaswa mara zote kuchagua namna inayowezekana iliyo na uwezekano mdogo zaidi wa kutengwa. Kutengwa kwya kawaida ka upumuaji, kwa mfano, kunaweza kuwa kuvaa kichuja hewa husika mpaka matibabu yako yatakapoleta mabadiliko na TB yako iwe haiwezi tena kuambukiza. Hutakiwi kuagizwa kukaa hospitali ikiwa kuvaa kichuja hewa kunatosha.

Katika baadhi ya hali nadra, serikali yako inaweza kukutaka ukae ukiwa umetengwa hata kama hauafiki (kutengwa bila hiari). Hii inaweza kutokea pale tu ambapo TB yako inaweza kuambukiza sana, ikiwa utakataa kutumia dawa za TB au kufuata njia za kudhibiti maambukizi, na kama kuna hatari yoyote ya kueneza TB kwa wengine. Kutengwa pasipo hiari hakutakiwi kufanywa kila wakati na kunapaswa kutumiwa tu ikiwa njia nyingine zote, ikijumuisha ushauri wa muda mrefu, zimetumiwa na kukosa kufanikiwa. Kutengwa pasipo hiari kunapaswa kuzingatia sheria na sera zilizopo, na kunapaswa kufanyiwa mapitio ya nje. Wewe kama mtu uliyeathirika una haki pia ya kupinga uamuzi wa kutengwa. Hupaswi kutengwa katika mandhari yasiyo ya kimatibabu, kama vile gerezani. Pia, unatakiwa kupewa matibabu ya TB na mahitaji muhimu, ikijumuisha chakula, maji na fursa ya kuwasiliana na familia yako. Kutengwa kunatakiwa kuwe kwa muda mfupi iwezekanavyo, ikimaanisha kuwa ili mradi tu TB yako inaambukiza na inaweza kuwa na hatari kwa wengine. Kutengwa hakutakiwi kuhitajika ili upewe dawa mpya za TB.

Je, Haki ya Faragha inamaanisha nini kwa watu walioathirika na TB?

Haki ya Faragha inamaanisha kwamba hali yako ya afya, ikijumuisha ikiwa una TB, na taarifa zako binafsi hazitakiwi kushirikishwa kwa yeyote, isipokuwa umeruhusu au ni muhimu ili kulinda afya za wengine. Katika sehemu nyingi, TB ni "hali inayolazimu kujulishwa". Hii inamaanisha kwamba mamlaka za afya zinapaswa kuripoti masuala ya TB kwa idara ya afya ya taifa. Hata hivyo, taarifa zako binafsi (kama jina lako) halitakiwi kushirikishwa. Ikiwa una watoaji tofauti wa huduma za afya, wanaweza kuhitaji kushiriki taarifa kuhusu afya yako na kati yao ili kukupa huduma za kiwango kizuri. Ikiwa TB yako inaambukiza na watu unaoingiliana nao wako katika hatari ya kupata TB, unapaswa kuwataarifu, kuwatia moyo wakapimwe na kuchukua hatua kujilinda dhidi ya usambaaji wa TB. Kwa mfano, unaweza kuchagua kuvaa kichuja hewa kinachostahili katika mazingira yaliyofungwa ya familia. Mtoaji wako wa huduma za afya anaweza kuwataarifu watu walio karibu nawe kuwa wanahitaji kupimwa, pasipo kutambua yupi yuko karibu. Ikiwa utakataa au huwezi kufanya hivi, mtoaji wako wa huduma za afya anaweza kuwataarifu watu hawa kuwa TB yako inaambukiza ili wachukue hatua ya kujilinda. Ikiwa hakuna hatari ya watu wengine kupata TB, Haki yako ya Faragha inapaswa kulindwa kabisa.

Je, Haki ya Sayansi inamaanisha nini kwa watu walioathirika na TB?

Haki ya Sayansi inamaanisha kwamba kila mtu anatakiwa kufaidika kutokana na matokeo mapya ya tafiti za kisayansi, ikijumuisha njia mpya na zilizoboreshwa za uzuiaji, utambuzi na matibabu. Serikali

yako inapaswa kuchukua hatua kuwezesha matibabu mapya, njia mpya za kuzuia TB, na njia mpya za kupima TB zipatikane nchini mwako. Serikali pia zina wajibu wa kusaidia na kuendeleza sayansi. Hiyo inamaanisha, kwa mfano, kwamba serikali yako inapaswa kutoa pesa kwa ajili ya utafiti wa kisayansi na kusaidia taasisi za umma za utafiti. Serikali yako inapotoa pesa ama ruzuku nyingine kwa ajili ya utafiti kwa kampuni binafsi, inapaswa pia kuhakikisha kwamba matokeo ya utafiti huo yanawanufaisha watu wenye TB katika nchi yako na ni ya gharama nafuu. Haki ya Sayansi inahusiana pia na haki ya kushiriki. Jamii zilizoathiriwa na TB zinatakiwa kuhusishwa kwenye mchakato wa utafiti katika hali ya heshima na yenye mantiki.

Je, Haki ya Taarifa ina maana gani kwa watu walioathirika na TB?

Haki ya taarifa ina maanisha, kati ya vitu vingine, kwamba wewe—na, ikiwa utapenda, mtu anayehusika katika uangalizi wako, kama vile ndugu au rafiki—anatakiwa kuambiwa kuhusu chaguzi zako za matibabu. Pia inamaanisha kwamba wewe na jamii yako mnapaswa kupewa taarifa sahihi kuhusu jinsi TB inavyosambaa, jinsi ya kuzuia kusambaa kwake, na kwa muda gani watu wenye TB wanaweza kuwaambukiza wengine. Unapaswa pia kupokea ushauri na maelezo yote unayohitaji ili kutoa idhini (kukubali) juu ya njia yoyote ya matibabu. Pia inamaanisha kwamba unayo haki ya kujua majina na dozi za dawa yoyote au matibabu ambayo daktari wako anataka utumie, kujua matibabu yatachukua muda gani, na kufahamu athari zote na namna nyingine ambazo matibabu au dawa zinaweza kuathiri afya au maisha yako. Huu unaitwa uelewa wa matibabu. Haki ya taarifa pia inamaanisha kwamba unapaswa kupokea nakala ya rekodi ya matibabu yako ikiwa unaihitaji.

Je, Haki ya Ridhaa ya kutaarifiwa inamaanisha nini kwa watu walioathirika na TB?

Haki ya Ridhaa ya kutaarifiwa inahusiana wa karibu na Haki ya Taarifa na Haki ya Kushiriki. Ridhaa ya Kutaarifiwa inamaanisha kwamba unatakiwa ukubali mbinu yoyote ya kimatibabu kabla haijafanyika, na kwamba unatakiwa kwanza upate taarifa kamili kuhusiana na athari na faida za njia hiyo. Taarifa ni msingi wa maamuzi yako ikiwa utaruhusu njia ya matibabu (kwa mfano, kanuni maalum za dawa za TB, au ikiwa unataka kutumia matibabu ya uzuiaji au la). Hii inamaanisha kwamba mara zote unapaswa kupata ushauri kabla hujafanya maamuzi, na kuwa unatakiwa upewe muda kufikiria kuhusu maswali na kupokea majibu ya maswali yako. Matibabu ya lazima hayaruhusiwi kabisa.

Je, Haki ya Kushiriki inamaanisha nini kwa watu walioathirika na TB?

Haki ya Kushiriki inamaanisha kwamba wewe kama mtu mwenye TB unatakiwa ushiriki katika maamuzi yanayokuhusu. Hiyo, bila shaka, inajumuisha matibabu yako . Lakini, pia ina mipaka ya utekelezaji wake. Watu walioathiriwa na TB wanayo haki ya kushiriki katika kuamua sera za afya, kutoka ngazi ya taifa mpaka ngazi ya jamii. Kwa mfano, hii inaweza kumaanisha kwamba mamlaka za afya zitatafuta michango kutoka kwa mashirika yanayowawakilisha watu wenye TB zinapotathmini miradi ya TB, au kushirikisha jamii katika kuendeleza njia itakayotumiwa katika eneo husika kwa huduma zinazomzunguka mtu.



Picha Inamlikiwa na: David Harrison kwa ajili ya Kampeni ya Shughuli za Matibabu

Je, Uhuru wa Kuungana na Uhuru wa Kukusanyika unamaanisha nini kwa watu walioathirika na TB?

Haki ya Kushiriki ni sababu mojawapo ya kuhusiana kwa Uhuru wa Kuungana na Kukusanyika naTB. Uhuru wa Kukusanyika unaruhusu makundi ya watu kuja pamoja, kwa mfano kujadili michango katika maswala ya afya ya jamii. Uhuru wa Kuungana unakuruhusu wewe na watu wengine walioathiriwa na TB kuanzisha na kusajili mashirika (kwa mfano, makundi ya kijamii yanayotoa msaada kwa watu walioathiriwa na TB) au kutetea haki za watu wenye TB.

Je, Huduma zinazomlenga mtu ni kitu gani?

Huduma zinazomlenga mtu ni kila kitu kinachohusu uzuiaji, utambuzi na matibabu ta TB vinapaswa kumzingatia mtu kwa ujumla wake. Hii inajumuisha kuheshimu haki za binadamu za kila mtu na kufikiri kuhusu vigezo vya kijamii na kiuchumi, sio tu kuhusu taarifa za matibabu. Mpango wako wa matibabu unapaswa kufanywa ili kushughulikia hali yako mahsusi. Unapaswa kulinda haki zako, sio kuzikiuka. TB inaathiri zaidi ya mtu mmoja. Hiyo ndiyo sababu tunafikiria kuhusu huduma zinazoilenga familia, na jamii pia. Watu wanaosaidia kuwahudumia wanafamilia na wanajamii wanaoishi na TB wanahitaji kutaarifiwa kuhusu uzuiaji, utambuzi na matibabu kama mtu mwenye TB anavyofanya.

Hii inamaanisha nini kwa familia na jamii?

Familia na jamii zina mchango muhimu katika uzuiaji, utambuzi na matibabu ya TB. Hiyo ndiyo sababu Mashirika ja Kijamii (CBO) na makundi ya kutoa misaada ni muhimu. Una haki ya Uhuru wa Kuungana na Uhuru wa Kukusanyika. Hii inamaanisha kwamba wewe, wagonjwa wengine na jamii yako mnayo haki ka kukutana na kushirikishana taarifa. Mnayo haki ya kuanzisha mashirika yanayowasaidia watu wenye TB, wahudumu wao na jamii zao.

Ninaweza kufanya nini ikiwa haki zangu zinakiukwa?

Una haki ya kutoa malalamiko. Mamlaka za afya zinapaswa kuwa na mfumo ambao utakuwezesha wewe kutoa malalamiko. Pia unayo haki ya kupokea majibu. Ikiwa hutapokea majibu, au ikiwa utapokea majibu ambayo hayashughulikii wasiwasi au mahitaji yako, una haki ya kuwashtaki mahakamani. Hii inategemea sheria za nchini mwako, na unapaswa kuwasiliana na mtaalamu wa sheria au mashirika ya usaidizi wa kisheria. Kuna mashirika yanayoshughulikia kwa njia mahsusi masuala ya ukiukaji wa sheria ya haki za afya. Hii inajumuisha yaki zako za kupata matibabu, kwa mfano, na haki zingine zilizoainishwa kwenye Sehemu ya I, "Haki zako za Kibinadamu na TB".

Nchi nyingi zina wachunguzi wa haki za binadamu au taasisi za kitaifa za haki za binadamu. Haya ni makundi yanayojitegemea yaliyopo ili kukagua, kulinda na kurejesha haki za binadamu na yanaweza kupokea malalamiko kutoka kwa watu kuhusu ukiukaji wa haki za binadamu. Unaweza kuchunguza ikiwa nchi yako ina taasisi ya kitaifa ya haki za binadamu kwa kuangalia saraka hii: https://nhri.ohchr.org/EN/Pages/default.aspx. Wakati mwingine, inaweza kuwa haraka kuwasiliana na shirika la utetezi wa kisheria kwa wagonjwa ikiwa unafikiri kwamba haki zako zimekiukwa na unataka kupata taarifa juu ya mapendeleo yako.